# OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

SHULE YA SEKONDARI KABASA,
S.L.P. 169,
**BUNDA.**

Kumb. Na. KBSS/J1/F.69/17 15/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI______________________
S.L.P.________________________
**BUNDA.**

**Yah: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KABASA HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA MKOA WA MARA MWAKA 2021</u>**

1. Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule ya Sekondari Kabasa. Hongera sana.
2. Shule hii ipo Kata ya Kabasa Tarafa ya Serengeti Wilaya ya Bunda, na ni ya Kutwa na ni ya mchanganyiko wa wavulana na wasichana.
3. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2020 kwa ajili ya Usajili na English Course na mwisho wa kuripoti ni tarehe 29/01/2021
4. **Sare za Shule**
   (i) Suruali mbili kwa wavulana, mifuko miwili pembeni na moja nyuma. Suruali isiwe ya modo. Rangi ya kitambaa ni damu ya mzee.
   (ii) Sketi mbili za damu ya mzee kwa wasichana, sketi ziwe ndefu zinazokaribia kisigino.
   (iii) Shati mbili nyeupe mikono mifupi kwa wote.
   (iv) Soksi nyeupe jozi mbili kwa wavulana na wasichana.
   (v) Tai damu ya mzee na pini zake. Jozi mbili kwa wote wavulana na wasichana.
   (vi) Jozi za viatu vyeusi vya ngozi kwa wote. Viwe vya kamba.

5. **Sare za Michezo**
   (i) T – shirt ya bluu na bukta kwa wote.
   (ii) Jozi moja ya viatu vya raba za michezo
   (iii) NB: Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule.

6. **Vifaa vya Shule anavyotakiwa kuja navyo**
   (i) Madaftari makubwa 12 yawe Counter book
   (ii) Mathematical set (Bofa) 1
   (iii) Kalamu nyeusi/bluu za wino, penseli na ufutio
   (iv) Dictionary moja English to English bila kuwa nayo mtoto hatapokelewa
   (v) Rula

7. (i) Mahindi yaliyokobolewa debe moja

(ii) Maharage kg 3
(iii) Chumvi ½ kg
(iv) Pesa ya mpishi 1,500/= kwa mwaka
(v) Pesa ya walimu wa muda (Part time teachers) na remedial – 10,000/= kwa mwaka

**NB: Michango ya fedha yote ilipwe kupitia Bank ya NMB Account No. 30102300497. Jina la Account ni Kabasa Sekondari Uzalishaji**

8. **Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo muhimu yaliyoelezwa hapa chini:-

(a) Heshima kwa Viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu siku zote za masomo.
(c) Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni (Preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(h) Ni lazima kila mwanafunzi afahamu kuwa lugha ya kufundishia ni Kiingereza isipokuwa katika somo la Kiswahili tu. Muda wote wasiliana na walimu wako na wanafunzi wenzako kwa lugha ya Kiingereza tu.
(i) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria Baraza la Shule, ukaguzi wa usafi na kupandisha bendera ya Taifa.
(j) Mwanafunzi huruhusiwi kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni (Guest House).
(k) Ni marufuku kuendesha baiskeli ndani ya eneo la ukakamavu shuleni. Eneo la ukakamavu linaanzia geti kuu unapoingia shuleni na kuishia geti kuu unapotoka shuleni.
(l) Ni marufuku kutembelea sehemu zifuatazo bila kibali maalumu na kazi rasmi
    a. Ofisi za shule
    b. Maabara
    c. Chumba cha walimu
    d. Nyumba za wafanyakazi
(m) Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu na kujali
    a. Wimbo wa Taifa
    b. Nembo ya Taifa
    c. Fedha ya Taifa
    d. Picha za Viongozi wa Taifaletu
(n) Kila mwanafunzi aweze kuimba nyimbo zifuatazo kwa ufasaha na heshima

a. Wimbo wa Taifa
b. Wimbo wa Tanzania Tanzania
c. Wimbo wa Shule
d. Tazama Ramani

(o) Huruhusiwi kufuga ndevu, nywele na kucha
(p) Unapaswa kutunza mali za umma

9. **Makosa yatakayoweza kusababisha kufukuzwa shule**

(i) Wizi
(ii) Uasherati na Ushoga
(iii) Ubakaji
(iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli, pombe, sigara n.k
(v) Kupigana na kupiga
(vi) Kuharibu kwa makusudi mali za umma
(vii) Kudharau Bendera ya Taifa
(viii) Kuoa au kuolewa
(ix) Kupata mimba na kuharibu mimba ndani ya shule ukiwa mwanafunzi.
(x) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule
(xi) Kukataa adhabu kwa makusudi uliyopewa na Mkuu wa Shule, mwalimu au kiranja.
(xii) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni
(xiii) Udanganyifu katika mitihani
(xiv) Kukwepa kufanya majaribio ya kila mwezi na mitihani yote
(xv) Matumizi ya lugha chafu kama kutukana na kukashifu
(xvi) Kutohudhuria vipindi darasani (utoro)

**NB:** Pamoja na barua hii imeambatanishwa na nyaraka zifuatazo:-

(i) Fomu ya kupima Afya (Medical Examination Form)
(ii) Ahadi ya mzazi na mwanafunzi juu ya utii wa sheria kanuni na taratibu za shule.

Fomu hizi zoteziletwe siku ya kufungua shule na kuwa mtoto hatapokelewa kama hatakuja nazo.

Nakutakia maandalizi mema.
KARIBU SANA

*Petro J. K*
MKUU WA SHULE
0783 – 471 183

MKUU WA SHULE
SEKONDARI YA KABASA
BUNDA

# HOSTEL

**HONGERA SANA!**
Mwanao ni miongoni mwa wanafunzi wachache wa kike walio bahatika kupata nafasi ya kuishi hostel Kabasa Sekondari. Shule inayo mazingira na huduma bora kabisa ya Hostel kwa wanafunzi wa kike ili kutimiza ndoto zao za kitaaluma, kijamii na hata kiuchumi.

**Huduma zinazotolewa kwa wanafunzi**

(a) Malazi bora kabisa
(b) Maji safi
(c) Malezi bora kwa wanafunzi wa kike (chini ya Matron na walimu)
(d) Umeme wa gridi ya Taifa
(e) Malezi ya Kiroho
(f) Masomo ya jioni, usiku na alfajiri (ambayo ni ya lazima)
(g) Ulinzi upo wakati wote.

**Mahitaji ya Hostel**
Chakula

(a) Mahindi debe 6 kwa mwaka
(b) Maharage kg 60 kwa mwaka
(c) Mchele kg 30 kwa mwaka

**NB**: Kila kimoja kitalipwa kwa awamu nne kwa mwaka

**Ada**
Ada ya Hostel ni Tsh. 155,000/= kwa mwaka. Fedha zote zitawekwa kwenye account Na. 30102300497, NMB Jina la account ni Kabasa Sekondari Uzalishaji mali. Ada hii ilipwe walau wiki moja kabla ya kuripoti shule kwa ajili ya maandalizi.
Ada italipwa kwa awamu nne kwa mwaka kama inavyoonekana hapa kwenye jedwali:-

| **Muhula wa kwanza** | | **Muhula wa Pili** | |
|---|---|---|---|
| Awamu ya I | Awamu ya II | Awamu ya I | Awamu ya II |
| 45,000.00 | 35,000.00 | 40,000.00 | 35,000.00 |

Matumizi ya ada ni kwa ajili ya:-

- Taaluma - nyama/dagaa - maji - umeme
- Matron - mafuta - chumvi - mlinzi
- Mpishi - kuni - sukari - tahadhari

**Mahitaji mengine**

- Ream moja ya karatasi
- Vazi la kushindia; gauni pea mbili kunguru rangi ya damu yam zee lishinwe solo.
- Vifaa vya michezo (raba, truck suit, T-shirt, skin tight)
- Shuka pea mbili za pink, mto na foronya, chandarua
- Ndoo moja ya lita 10 kwa ajili ya usafi na chombo kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa.
- Vyombo vya chakula, bakuli, sahani pamoja kikombe na kijiko.
- Kandambili na taulo
- Dawa ya meno na mswaki
- Kanga/kitenge pea moja.
- Taulo za kike walau kuanzia tatu na pesa kidogo kwa ajili ya kujikimu.

**NB:** Aliye na bima ya Afya aje nayo kwa ajili ya kurahisisha matibabu. Na asiye na bima aje na Tsh. 6000/= kwa ajili ya kujiunga na bima ya Afya ya jamii.

# OFISI YA RAIS

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA**
**SHULE YA SEKONDARI KABASA**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA HULE**

1. Jina kamili (kama lilivyo kwenye TSM9)________________________________________
2. Anuani ya nyumba____________________________________________________________
3. Tarehe ya kuzaliwa____________________________________________________________
4. Mahali alipozaliwa, Kijiji__________ Kata___________ Tarafa________Wilaya__________
5. Mahali unapoishi kwa sasa________________________________________________
6. Shule ya Msingi/Sekondari ulikotoka____________________________________________
7. Dini/Dhehebu__________________________________________________________________
8. Kabila__________________________________________________________________________
9. Taifa (Mtanzania/Si Mtanzania)______________________________________________
10. Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu kwa masuala yahususyo shule (Ni lazima kujaza sehemu zote nne)
    a. Jina la baba__________________________________________ Simu_________________
       Anaishi/haishi_______________________ kazi yake__________ Anuani_____________

    b. Jina la mama_________________________________________ Simu_________________
       Anaishi/haishi_____________________ kazi yake__________ Anuani______________

    c. Jina la mlezi1.________________________ uhusiano_____________ simu__________
       Kazi yake__________________________________ Anuani__________________________

    d. Jina la mlezi2.________________________ uhusiano_____________ simu_________
       Kazi yake______________________________ Anuani______________________________

Mimi (mwanafunzi)_____________________________________________ nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu; Nakubai kwa dhati kanisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na Uongozi wa shule.

Saini ya mwanafunzi______________________________ Tarehe_________________

Mimi (jina la Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi)____________________________________ ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi____________________________________ nimeyasoma masharti ya Shule ya Sekondari Kabasa ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa. Aidha naahidi kushirikiana na Uongozi wa Shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadae awe raia bora mwema wa Taifa letu.

Saini ya Mzazi/Mlezi_____________________________ Tarehe___________________

**ZINGATIA: HATUPOKEI MWANAFUNZI SIKU YA JUMAMOSI NA JUMAPILI**

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

KABASA SECONDARY SCHOOL,
P.O.Box 168,
**BUNDA.**

**PART A: TO THE MEDICAL OFFICER**

Please examine the person below as to his/her physical and mental fitness for enrollment as a student. The examination should include the following categories:-

____________________________________________(name in full)

(i)

- (a) Eye – sight____________________
- (b) Hearing____________________
- (c) Limbs____________________
- (d) Speech____________________
- (e) Venereal disease____________________
- (f) Leprosy____________________
- (g) Epilepsy____________________

(ii) Neuroses____________________
(iii) Other serious diseases____________________
(iv) Pregnancy____________________

**HEAD MASTER**

MKUU WA SHULE
SEKONDARI YA KABASA
BUNDA

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

**(To be completed by a government Medical Officer)**

(i)

- (a) Eye – sight____________________
- (b) Hearing____________________
- (c) Limbs____________________
- (d) Speech____________________
- (e) Venereal disease____________________
- (f) Leprosy____________________
- (g) Epilepsy____________________

(ii) Neuroses____________________
(iii) Other serious diseases____________________
(iv) Pregnancy if applicable____________________

I have examined the above named person and consider that he/she is not physical and mentally fit for **SECONDARY EDUCATION**

Date______________ Name____________________ Signature____________

Station____________________ Designation____________________